MAELEZO SAHIHI

MUONGOZO WA REDIO

MUONGOZO WA SHUGHULI ZA KIJAMII

MASOKO, MAVAZI & MITINDO

TANZANIA

CHILDREN'S RADIO FOUNDATION

MYCN

UTANGULIZI

Mavazi yetu yanasema mengi kuhusu tunavyojitokeza ulimwenguni. Tunavaa ili kuwavutia wengine au kuonyesha hisia zetu binafsi. Mitindo (fashion) ni mfano mkuu wa jinsi wafanyabiashara hulenga hisia zetu (badala ya akili inayotoa maamuzi ya busara) ili kutushawishi na kututia tamaa ya urembo, utajiri na sifa - na kutuhimiza kuendelea kununua zaidi! Kununua kwetu huangazia kujifurahisha, sifa na burudani: Tunapofikia kununua mavazi, wengi wetu hufikiria tunachotaka zaidi kuliko tunachohitaji - na kuhusu kujionyeshana kwetu na sifa tutakazopata kuliko athari inayoletea Dunia - lakini matokeo ya athari kwa mazingira kutokana na mavazi yetu ni kubwa. Sekta ya mtindo ya mavazi ndio sekta ya pili kwa uchafuzi mkubwa duniani, ikifuata ile ya mafuta. Inachangia 10% ya uzalishaji wa gesi chafu duniani.

Kuongezeka kwa utandawazi wa kiuchumi katika kipindi cha miaka 50 iliyopitia imeibua sekta kubwa ya mitindo ya mavazi ulimwenguni kote. Zamani, mavazi yalikuwa hayapatikani kwa urahisi - na kuyapata ilikuwa ni kazi kubwa na yenye gharama kubwa ya rasilimali. Mavazi yalikuwa yakishonwa kwa mkono, kwa kutumia vyanzo vilivyo tokana na pamba, sufi za unyoya au fani (flax). Siku hizi, mavazi yetu mengi huzalishwa kwa wingi kupitia minyororo ya uzalishaji ya kimataifa: wakati tunaponunua nguo mpya, huwa tayari wafanyakazi 80 tofauti duniani kote wameshiriki katika michakato ya kukuza, kuvuna, usindikaji, kusafirisha, kutengeneza viwandani, kuchora na kushona ili tu kuzalisha ile nguo. Na hata hivyo, siku hizi nguo zinapatikana kwa wingi sana, na mara nyingi kwa bei nafuu, na watumiaji wengi huzichukulia kama bidhaa za kutupwa (disposable). Nchini Marekani kwa mfano, nguo za kike huvaliwa jumla ya mara saba tu kabla ya kutupwa.

TAFSIRI

- **Alama ya kikaboni ya bidhaa** - Kama vile una alama yako ya kikaboni kwa Dunia ambayo inatokana na shughuli zako zote za matumizi - pia vitu unavyotumia vina alama. Kwa mfano, mavazi zetu yanahitaji ardhi, maji na dawa za kuua wadudu ili kukuza ile pamba na nyuzi nyingine zinazotumika; au kiasi kikubwa cha kemikali za petroli na nishati asili za mafuta zinatumika ili kuzalisha vitamba vya kusandiwa (synthetic) kama nylon au polyester. Zaidi ya hayo, mafuta asili hutumika kusafirisha na kutengeneza vitambaa na mavazi, na kemikali zinazotumiwa katika mchakato wa kuzitia rangi - zote huchangia kwenye alama ya kikaboni. Kwa mfano, inachukua lita 2,700 za maji ili kuzalisha shati moja ya pamba, ambayo ni sawa na maji ya mtu mmoja ya kunywa kwa miaka 2 ½!
- **Mzunguko wa Maisha** - Mitindo ni mfano mkuu wa sekta ambayo inaweza na inastahili kutoka kwenye mzunguko wa uzalishaji wa mstari (ambapo nguo hutengenezwa, kuvaliwa na kisha kutupwa) na kuibadilisha kufukia kuwa mzunguko wa uzalishaji wa mviringo ambapo mavazi hutengenezwa kudumu kwa muda mrefu, wakitumia taratibu za kupunguza nishati na pembejeo za vifaa; kuvaliwa kwa muda mrefu, kutengenezwa wakati inapohitajika, na kisha kuchakatwa kutoa nguo mpya badala ya kutupwa kama taka. Inakadiriwa kuwa 85% ya nguo zinazopatikana sasa zinaweza kutumika tena, lakini katika nchi tajiri, ni 1% tu ya mavazi huchakatwa, na nguo nyingi zinafikia kutupwa katika mashimo makubwa ya taka ardhini, mara nyingi hata kabla kumaliza mwaka kutoka ziliponunuliwa.
- **Masoko** - ni vitu vyote ambavyo kampuni zinafanya kutambua na kukata rufaa kwa mahitaji yasiyotimizwa, na pia yale mahitaji

ya makundi ya wanunuzi wanaolengwa ili kampuni ipate faida (Heidi Cohen). Hii inamaanisha kuunda na kuendeleza bidhaa kupitia ujumbe ulio katika matangazo, alama za kutambulisha bidhaa na vyombo vya habari vya kijamii. Masoko huwa na jukumu kubwa katika kuendesha mitindo na mazoea yasiyoweza kudumu - kwa mfano kubadilisha mitindo 'kila mara na kwa kiasi kikubwa' ni aina ya mbinu iliyopangwa ili kuwahamasisha watu kununua zaidi - tuseme ni mwaka huu viatu vyenye mpindo vinafaa; lakini mwaka ujao viatu vya aina ingine tofauti vitatokezea kama mtindo mpya wa kutamaniwa.

- **Mitindo ya haraka** - Makampuni ya mavazi (kama H&M na Zara) huongeza mauzo yao kwa kuharakisha kalenda ya kawaida ya mitindo na kutoa mtindo mpya wa nguo za bei nafuu kila miezi michache (au hata kila wiki chache!). Nguo hizo hazijatengenezwa kudumu kwasababu mitindo hubadilika upesi, na pia kwa sababu ni za bei nafuu, na zimekosa ubora. Kwa mfano, kitambaa huwa chepesi, na kimeshonwa mara moja badala ya mara mbili. Wazalishaji hawa wanajua tu kwamba watu wengi watanunua vazi jipya badala ya kutengeneza lililopo.
- **Utandawazi** - Utandawazi wa uchumi kwa zaidi ya miaka 50 iliyopita una jukumu kubwa katika jinsi mavazi yetu yanavyozalishwa. Kabla ya utandawazi, mavazi yalichukuliwa kuwa bidhaa ya kifahari, na kwa kawaida yalitengenezwa kwa kutumia nyuzi, rangi na wafanyakazi wa ndani. Siku hizi, shati yako mpya (t-shirt) inaweza kuwa ilisafiri zaidi ya mara moja ulimwenguni kabla ya kukufikia wewe. Wakulima wa pamba huko Misri, Burkina Faso au Mexico; na wafanyakazi wanaoshona nguo nchini Cambodia, Bangladesh au China, wote wanaweza kuwa walishiriki katika kuzalisha shati lako. Katika uchumi wa dunia, sekta za mavazi zinazoshindana zinawezeshwa na mbinu ya biashara ya 'gharama ya chini, mshahara mdogo'. Hii ina maana kwamba shati mpya inaweza kuonekana kuwa ya bei nafuu kwako - lakini, kama tunavyoweza kuchunguza, wingi huu wa mavazi ya bei nafuu una athari kubwa kwa Dunia, hali ya mabadiliko ya tabia nchi na wafanyakazi wanaozalisha.
- **Soko wazi** - ni mpangilio wa kiuchumi ambao unahimiza uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa udhibiti mdogo wa serikali, na kuruhusu soko yenyewe kusimamia bei na usambazaji. Katika mfumo huu, wanaozalisha na wanaotoa bidhaa wana uhuru wa kuamua watakacho zalisha, na jinsi watakaoitumia. Katika mfumo ulio na udhibiti mdogo na unaolenga kuongeza faida, kuna hatari ya unyonyaji wa wafanyakazi na mazingira.
- **'Sweatshops'**- ni viwanda vinavyotengeneza mavazi na bidhaa nyinginezo, na ambako wafanyakazi hulipwa mshahara mdogo kwa masaa mengi, na kufanyia kazi katika hali duni. Bidhaa za kimataifa kama Nike, Adidas na H&M zimekashifiwa kwa kutumia 'sweatshops', na pia kutumia wafanyakazi watoto katika nchi zinazoendelea na sheria za wafanyakazi hazizingatiwi kwa makini. Kwa mfano, Bangladesh ambayo ina nafasi ya pili baada ya China ya kuuza mavazi kwa masoko ya nga'mbo, ndio nchi yenye ulinzi dhaifu zaidi wa wafanyakazi, na mshahara wa chini wa $0.41 tu kwa kila saa (Forbes). Mnamo mwaka wa 2013, kuanguka kwa jumba la Rana Plaza, kiwanda cha mavazi chenye gorofa nane nchini Bangladesh, iliwaua wafanyakazi zaidi ya 1,000, na hio ikawa ishara kwa wengi ya ukosefu mkubwa wa usawa katika biashara ya kimataifa ya mavazi.
- **Nguo za mtumba** - Kuna soko kubwa la nguo zilizotumiwa na mara nyingi zinatoka Ulaya na Marekani ya Kaskazini, ambako watu hutoa mchango wa mavazi. Zoezi hili limeleta nguo nyingi za bei nafuu kwa Afrika, na kuhifadhi nguo za zamani kutoka kwa mashimo makubwa na taka ardhini kwenye nchi za Magharibi. Lakini soko la mavazi ya mtumba lina utata kwa sababu zimechangia kwa watu kutonunua nguo kutoka kwa viwanda vya ndani. Serikali za Afrika Mashariki hata zinazingatia kupiga mitumba marufuku ili kuendeleza viwanda vya ndani vya nguo.
- **Mavazi yaliotengenezewa kwa njia ya maadili** - Wabuni mitindo Afrika na duniani kote wanajaribu njia tofauti za kuzalisha nguo zisizoathiri jamii na mazingira, kwa mfano kwa kuchakata na kuchapa nguo (yaani recycling and upcycling), kutumia nyuzi za asili zinazozalishwa kwa ustawi,

na kuzalisha vitambaa kutoka kwenye bidhaa za taka (kama vile: chupa za plastiki, vipande vidogo-vidogo vya vitambaa na ngozi, nyuzi za ndizi, maganda ya kahawa). Wanatumia kanuni za mviringo, na kukuza ufundi na viwanda vya ndani. Wabuni mitindo wanaokubali mwenendo huu wanazidi kujiondoa kutokana na mitindo ya haraka, na kuhakikisha wamebuni mavazi ya kudumu. Wanatumia vitambaa bora na mitindo ya kupendeza inayoweza kustaili kwa muda mrefu, wakishirikiana na wazalishaji wa ndani. Wabuni mitindo vijana wa Kiafrika wanaongoza mwenendo huu, kwa mfano, kwa kuzalisha mavazi ya kiasili yailiotengenezewa kwa mkono, na kuendeleza mila za kale za mavazi, kama vile uzalishaji wa nguo kutoka kwenye gome nchini Uganda (YouTube), ili kuwa rufaa kwa watumiaji wa kisasa.

ONDOA HADITHI POTOFU (UZUSHI)

UZUSHI	UKWELI
Mavazi yaliotolewa nchi za nje yana ubora na mitindo mizuri zaidi kuliko mavazi yatokayo nchini ndani	Mavazi yaliotolewa nchi za nje mara nyingi huwa mitindo ya haraka, inayozalishwa katika 'sweatshops' duniani kote na kwa gharama kubwa kwa mazingira. Upatikanaji wa mavazi ya bei nafuu yaliotolewa nje pia huumiza viwanda vya ndani ambavyo haviwezi kushindana na hali ya mishahara midogo na uchumi wa kuzalisha kwa kiwango kikubwa katika sekta ya mtindo ya kimataifa. Hata vitambaa vya Kiafrika kama vitenge hutengenezewa nchini China na kuuzwa kwa bei nafuu kuliko vile vilivyotengenezwa nchini. Mwelekeo huu unafuta urithi mkubwa wa mavazi tofauti ya Kiafrika ... Hata hivyo, wabunifu wa Kiafrika wanaozalisha kwa kiwango kidogo, kama studio 189 nchini Ghana, wanatambua utajiri ulio kwenye ubunifu wa kitamaduni, na kushirikiana na wataalamu wa ndani ili kuingiza mchakato wa kuska (weaving) na kutia rangi (batik) katika miundo.
Ninahitaji kununua nguo mpya kila mwezi, lakini haiathiri mazingira.	Ununuzi wa mavazi kila mwezi una athari kubwa kwa mazingira! Kiasi cha maji na nishati za mafuta, pamoja na matumizi ya madawa ya kuua wadudu ili kukuza pamba au vitu vingine, ikiwa ni pamoja na vya kuzalisha, ili kuzalisha vitambaa huongeza uchafuzi wa maji na mazingira duniani kote kutoka kwenye kemikali, rangi, dawa ya klorini na madini mazito.
Ninaweza kupunguza alama yangu ya athari duniani kwa kununua nguo za mtumba	Hii mara nyingi ni kweli, lakini pia unahitaji kuelewa mavazi yako ya mtumba yametoka wapi. Mitumba inaweza kuwa na alma nzito kuliko unvyofikiri, na inaweza pia kuwa inadhoofisha sekta ya mavazi nchini.

JE WAJUA? (KIDUNIA)

UZALISHAJI WA NGUO HUTOA ZAIDI YA TANI BILIONI ZA GESI CHAFU KWA MWAKA - KIWANGO KIKUBWA KULIKO CHA USAFIRI WA KIMATAIFA NA USAFIRI WA HEWA KIJUMLA

UZALISHAJI WA NGUO UMEONGEZEKA KWA MARA MBILI ULIMWENGUNI KATIKA MIAKA 15 ILIYOPITA, na zaidi ya nguo 100 billioni zilizalishwa duniani kote mwaka 2015 kutokana na kuongezeka kwa mitindo ya haraka na walio katika daraja la kati la mapato.



(Ellen MacArthur Foundation)

VAZI LA KAWAIDA LINALOVALIWA LEO LIMEHUSISHA WATU 80 TOFAUTI ULIMWENGUNI KUIZALISHA - IKIWA UTAHESABU UGAVI MZIMA - KUTOKA KWA WAKULIMA WANAOKUZA NYUZI, WAFANYAKAZI WA VIWANDA (SWEATSHOPS) NA WAUZAJI WA REJAREJA (ST. JAMES)

70% ya mito na maziwa ya Asia zinahofiwa kuwa na uchafu uliotokana na kemikali zilizopatikana katika galoni milioni 2.5 za maji machafu iliyotolewa kila mwaka na sekta ya nguo.

Robo ya kemikali za dunia hutumiwa katika uzalishaji wa mavazi, na kuifanya kuwa sekta ya pili kwa kuchangia uchafuzi wa maji, baada ya sekta ya kilimo cha viwanda



Katika nchi ambazo mitindo ya haraka hupatikana kwa urahisi, mnunuzi wastani hununua nguo 60% zaidi ya kuliko alivyofanya miaka 20 iliyopita, lakini anaweka kila vazi kwa nusu ya muda tu

JE WAJUA? (KIDUNIA)

UNAJUA KUHUSU TAKA ZA PLASTIKI NDANI YA BAHARI?

Nyingi ya plastiki hii hutoka kwenye nyuzi ndogo-ndogo za nguo za kusandiwa (synthetic) ambazo watu hufua katika mashine, na kusababisha chembechembe ndogo za plastiki kuingia kwenye mfumo wa maji na hatimaye bahari, zikichafua mlolongo wote wa chakula baharini na plastiki!



JE, WAJUA? (KWA NCHINI TANZANIA)

Kufuatia uhuru mwaka wa 1961, Tanzania iliwekeza zaidi katika sekta ya nguo. Ilikuwa imejitosheleza katika uzalishaji wa nguo, na kuchangia kwa kiasi kikubwa kwa ajira na Pato la Taifa, hadi uchumi uliposhuka na kukawa na uhuru wasoko miaka ya 1980 na 90.



(Tanzania Gateway)

Tanzania inaingiza vipande milioni 540 vya mavazi yaliotumika kila mwaka kutoka nje (ijulikanayo kama mitumba), ikilinganishwa na vipande milioni 20 vya nguo zinazozalishwa ndani ya nchi, na vipande milioni 177 vya nguo zilizoagizwa.

(ODI, 2017)

JE, WAJUA? (KWA NCHINI TANZANIA)

Mwaka 2015, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilitangaza mpango wa kuondokana na kuiingiza mitumba kutoka nchi za nje ifikapo 2019, kwa jitihada za kupanua viwanda vya ndani vya mavazi. Madhara ya mitumba kwenye uchumi wa ndani ni ngumu na yenye utata: kwasababu kwa upande mwingine, biashara ya mitumba hutoa ajira kwa wafanyabiashara wa ndani, pamoja na nguo za bei nafuu kwa wananch



Mahitaji ya mavazi yanakuwa kwa kasi nchini Tanzania kuliko nchi nyingine nyingi zinazoendelea. Hii inaweza kuimarisha mahitaji ya kimataifa kwa mara tatu zaidi ya leo, ifikiapo 2050. Bila mabadiliko makubwa, sekta hiyo itatumia **26% ya bajeti ya kimataifa ya kaboni** inayohusishwa na digrii **2 ya kupanda kwa kiwango cha joto duniani**.



(Ellen MacArthur Foundation)

Biashara ya kimataifa ya mavazi, pamoja na mazoea ya kunyonya wafanyakazi na kufanya biashara ya uchumi wa kiwango kikubwa, huleta vikwazo vikuu kwa vijana wabunifu wa Kiafrika wanaotaka kuzalisha viwango vidogo vya mavazi yaliyotengenezwa kwa njia inyozingatia maadili, ndani ya nchi. Kwa mfano, mishahara midogo katika biashara ya kimataifa huweka shinikizo kwa viwanda vya Afrika vya ndani kuufuata mtindo huo:

kushindana na wafanyakazi wa viwanda vya mavazi yenye mishahara ya chini huko Cambodia na Bangladeshi, kwa mfano, wafanyakazi wa viwanda vya mavazi nchini Ethiopia wanapata $20 tu kwa mwezi.



KUCHUNGUZA UWEZO WA SEKTA YA MITINDO NA MAVAZI YA KUKUZA MAENDELEO ENDELEVU AFRIKA

Kama sekta ya uumbaji iliyojengwa na makampuni ya biashara ndogo-ndogo na za wastani zinazoajiri wanawake na vijana, sekta ya mitindo Afrika ina uwezo mkubwa wa kutoa ajira na kuchangia uendelevu na maendeleo katika mlolongo wa thamani.
18% ya pamba ya dunia inazalishwa Afrika, na kuna uwezekano wa kukuza mlolongo wa thamani wa pamba, ikiwa ni pamoja na uzalishaji, kuchapisha, kusuka, kutia rangi, na ubuni. Pia itakuwa bora kwa mazingira, kwasababu kiasi kikubwa cha pamba kitazalishwa na kilimo cha mvua, kuvunwa kwa mkono na kuzalishwa kwa njia isiyotumia kemikali nyingi.

Vijana wengi ambao ni wajasiriamali wa mitindo wa Kiafrika wanaelekea kwenye mfumo wa uzalishaji wa mviringo na kuchakata, na kushirikisha mbinu za kitamaduni za nguo - ustadi na ubunifu wao unaweza kuendeleza mitindo inayodumu kwa muda mrefu na yakupendeza:

- **Zuri** ni alama ya bidhaa kutoka Kenya ambayo hutoa vitambaa vyake kutoka kwa wazalishaji wa Afrika Mashariki na hushirikiana na wataalamu wa mitaa na mafundi wenye ujuzi wa ndani, ili kuzalisha mavazi kutoka kwenye vitambaa vyenye rangi ya kuvutia vilivyochapishwa.
- **Mayamiko**, nchini Malawi, hutoa ajira kwa wanawake wanaotumia usanii wa kitamaduni wa kugeuza vipande vya vitambaa kuwa shodo (sanitary pads) ambazo zinaweza kuchakatwa, na shodo hizo kutolewa kama mchango kwa wasichana nchini.
- **Osei-Duro** huzalisha vitambaa na kuzigeuza kuwa mavazi maridadi nchini Ghana, Peru na India, wakishirikianai na wataalamu na wasanii wa ndani, kwa kutumia mbinu za kitamaduni ikiwa ni pamoja na batik za Afrika Magharibi, kutia rangi ya mimea, uchapishaji na uchoraji wa mkono.

UNAFIKIRIAJE?

- Nyingi ya mipango hii inalenga masoko ya juu ya Ulaya na Marekani ya Kaskazini, ambako wanajua watumiaji wa kimaadili walio na mapato ya juu wako tayari kununua bidhaa za mtindo wa polepole.
- Unafikiriaje kuhusu miradi kama hii? Je, inaweza kusaidia kupunguza athari kutokana na sekta ya mitindo, au hii tu ni njia ya kugeuza mitindo ya kimaadili kuwa ya kifahari?

RASILIMALI

- Ethical fashion in Ghana: Mitindo ya kiadili nchini Ghana: https://www.youtube.com/watch?v=_xbV5_W0XyY&feature=youtu.be
- Donated clothing threatens Kenyan textile industry (AP)· Mavazi yaliyotolewa (mitumba) yanayohatarisha sekta ya nguo za Kenya (AP) https://www.youtube.com/watch?v=hkyFhvXNKH8&feature=youtu.be
- 7 facts about how fashion harms the environment: Ukweli 7 kuhusu jinsi mitindo inavyoathiri mazingira https://www.facebook.com/worldeconomicforum/videos/798634890510096/
- East Africa Community to ban second hand clothes imports · Jumuiya ya Mashariki ya Afrika imepiga marufuku biashara ya kuleta mitumba kutoka nga'mbo https://www.youtube.com/watch?v=kTUU16xi-tw
- The second lives of old clothes· Maisha ya pili ya nguo za mtumba https://www.youtube.com/watch?v=kTUU16xi-tw
- Senegal's second-hand clothing boom· Sura ya pili ya nguo za mtumba nchini Senegal https://www.youtube.com/watch?v=BStentz20Rw
- Is fast fashion destroying the environment?· Mitindo ya haraka zinaharibu mazingira? https://www.youtube.com/watch?v=YOA0D0i5-fA
- The problem with fast fashion· Tatizo la mitindo ya haraka https://www.youtube.com/watch?v=iq0--DfC2Xk

MASOKO, MAVAZI & MITINDO
MUONGOZO WA KIPINDI CHA REDIO

MAANDALIZI YA KIPINDI

MADA MAHUSUSI

NJIA TOFAUTI ZA KUZUNGUMZA KUHUSU MASOKO, MAVAZI NA MITINDO

- Jamii inyoasaidia kuweka thamani na kujifunza mbinu za kutengeneza mavazi kwa mikono
- Fikiria kuhusu alama ya athari zilizotokana na mavazi yako binafsi kutoka wakati wa kuzaliwa hadi sasa. Inaonekanaje?
- Mavazi yaliotengenezewa ndani kwa njia ya maadili. Hizi zinapatikanaje katika jamii yako?
- Viongozi wa vyombo vya habari vya kijamii: Je, wanaathirije maamuzi yetu ya ununuzi wa mavazi au bidhaa za aina fulani?
- Mzunguko wa maisha wa mavazi. Kutoka kwa mbegu hadi ifikiapo kutupwa kwa shimo kubwa la taka kwenye ardhi.
- Ni ishara gani hukuonya kwamba vazi fulani ni la mtindo wa haraka/kuharibu ardhi/kuathiri watu?

CHAGUA MADA MAHUSUSI

Viongozi wa vyombo vya habari vya kijamii (social media influencers): Wanathiri aje maamuzi yetu ya ununuzi wa mavazi au bidhaa za aina fulani?

Njia za kuzungumza kuhusu: Viongozi wa vyombo vya habari vya kijamii: Je, wanaathirije maamuzi yetu ya ununuzi wa mavazi au bidhaa za aina fulani?

- Viongozi wa vyombo vya habari vya kijamii (social media influencers) hushawishi tamaa yetu ya mitindo ya haraka.
- Je, kiongozi aliyewajibika hufanyaje? Ni nini haswa anasaidia kuuza?
- Kupenda kwetu kwa vitu - na shida inayoletea mazingira: vyombo vya habari vya kijamii na viongozi wa vyombo hivyo wanaweza kufanyaje?
- Vyombo vya habari vya kijamii ni chombo cha biashara kwa viongozi hao. Wasipouza mavazi na bidhaa, nao watatoa kipato chao wapi?

MIUNDO YA VIPENGELE VYA KIPINDI

SAUTI ZA UMMA

Lengo la sauti za umma
Kupata maoni mengi kuhusu mada moja.

Utazungumza na nani
Mtu yeyote kutoka kwa jamii

Swali
Mtindo uliochakatwa ni nini?

MAONI YA SAUTI

Nia ya maoni ya sauti
Kupata maoni ya watu kuhusu mada ambayo wanaijali.

Utazungumza na nani
Uliza mfanyabiashara ya mavazi katika jamii ikiwa atajisikia huru kuzungumzia uzalishaji wake.
AU
Uliza kijana azungumzie uhusiano wake na mavazi.
AU
Uliza mtu mzee azungumze kuhusu alivyoona mabadiliko ya mitindo na masoko.

WASIFU WA SAUTI

Lengo la wasifu wa sauti
Wasikilizaji wasikie hadithi ya kuhamasisha kuhusu mada ya kipindi.

Unazungumza na nani
Mmiliki au mfanyabiashara ya mavazi katika jamii ambaye anaweza kuzungumzia uzoefu wake wa kununua au kuuza mavazi. Au unaweza kumhoji mtu anayechakata au kupakia nguo katika jamii yake.

Maswali

- Je, unadhani kwamba viwanda na uuzaji mavazi kunaathiri mazingira? Vipi?
- Unafanyaje ili kupunguza athari inayotokana na biashara yako?
- Kwa maoni yako, ukoje upatikanaji wa mavazi yaliyotengenezwa ndani au katika eneo lako?
- Wanunuzi wanahitaji kufikiria kuhusu mambo gani kabla ya kuchagua kununua mavazi?

Tafadhali angalia maswali ya mahojiano katika sehemu ya “Jinsi ya kuandaa kipindi chako”.

TANGAZO LA UMMA

Lengo la tangazo la umma
Kuweka mwamko wa jamii kuhusu jambo fulani.

Unda Tangazo la Umma linalosaidia watu kuelewa jinsi ambavyo tabia zao za matumizi kote duniani huchangia kuongezeka kwa kiwango cha joto duniani.

Kwa mfano
Sauti 1: Hey Jabu, umeona ile simu mpya? Yoh yoh yoh ni poa sana, na hakika mini nit-ainunua wiki ijayo.
Sauti 2: Eish Zibele, mara una simu nzuri kabisa kwa nini tena unataka mpya?
Sauti 1: Ah! Jabu, haina wasiwasi. Niko kwenye mradi na ni wakati wa kujiboresha. Ninahitaji kujipiga selfies bora pia, unaoona. Simu mpya! Mimi mpya!
Sauti 2: Na utafanya nini na ile simu ingine yako sasa ambayo iko katika hali kamili? Utatumia simu mbili sasa?
Sauti 1: Hapana Nitaweka moja tu kama akiba, unaoona.
Sauti 2: Hapana, Zibele. Huo ni uharibifu. Unajua ni kiasi gani cha nishati na rasilimali inachukua kutengeneza simu moja tu? Ili tu upate nyingine kwa miaka miwili. Umesikia kuhusu uzalishaji wa gesi chafu? Wewe mwenyewe sasa unazichangia!

Kauli mbiu
Tabia za utumiaji huathiri mabadiliko ya tabia nchi. Chakula, nguo, simu na vitu vingine tunavyonunua -zinachangia 60%ya gesi chafu duniani. Usiwe mtumiaji asiyejali. Fikiria kabla ya kununua!

JINSI YA KUANDAA KIPINDI CHAKO

Tumia miundo ya vipengele vya kipindi cha redio, utafiti wako na maandalizi yaliopendekezwa ili kuunda kipindi chako.

[MWANZO:]
Mtangazaji 1: Imetimia [TAJA SAA] na karibu ujiunge nasi kwenye makala ya [TAJA JINA LA KIPINDI] hapa [TAJA JINA LA STESHENI] . Mimi ni [TAJA JINA LAKO].

Mtangazaji 2: Hiyo ni kweli! Na jina langu ni [TAJA JINA LAKO], na kwenye kipindi cha leo tutazungmza kuhusu masoko, mavazi na mtindo, na jinsi sekta ya mavazi inavyoathiri mabadiliko tabia nchi! Ndio, marafiki zangu, mliisikia. Tutazungumzia kuhusu jinsi vijana wanaweza kupunguza kuchangia kwao kwa uharibifu wa mazingira kwa kuwa na ufahamu wa ununuzi wa mavazi yao.

Mtangazaji 1: Hiyo ni kweli, tutazungumzia pia kwa nini ni muhimu sana kwamba vijana, na watu wote, wazingatie jinsi wanavyojali nguo, kutoka wakati wanapozinunua hadi wanapozichoka na kuzitupa. Mahitaji ya nguo kwa Watanzania yanakuwa kwa haraka sana. Bila mabadiliko katika tabia zetu kama watumiaji, sekta ya nguo inaweza kutumia hadi 26% ya bajeti ya kaboni duniani kwa mwaka wa 2050.

Mtangazaji 2: Wow! Hiyo ina maana kwamba tunachangia 2% kwa kuongezeka kwa kiwango cha joto ulimwenguni. Sio poa! Leo, tutaangazia watu wanaonunua, kuuza na kuvaa mavazi katika jamii yetu. Karibu kila mtu huvaa nguo, lakini ni wangapi wetu wanaofahamu safari ambayo mavazi haya yamepitia ili kutufikia? Na ni wangapi wetu wanaofikiria kuzitupa kwa njia isiyo athiri ardhi wakati hatutazitaka au kuzihitaji tena? Ili kufanya hivyo, tunashirikisha sauti za jamii yetu kutuambia jinsi vyombo vya habari vya kijamii, matangazo na bidhaa zinavyotumiwa na watu wote, vijana kwa wazee, katika maisha yetu ya kila siku. Tunakuletea habari zinazohitajika ili kuanza mazungumzo ya wazi kuhusu masoko, mavazi na mitindo.

Mtangazaji 1: Hebu tujisikie zaidi kuhusu kile ambacho watu wanafikiri kuhusu masoko, mavazi na mitindo.
[TAJA ANAYEHOJIWA]
[CHEZ MAHOJIANO]

[KUFUNGA KIPINDI]
Mtangazaji 1: Leo tumejifunza mengi kuhusu masoko, mavazi, mitindo na njia endelevu za watu wote kushirikiana na mavazi yao!

Mtangazaji 2: Naam! Kuelewa alama yako ya mitindo ni muhimu sana kwetu vijana ili kutuwezesha kufanya maamuzi na mipango mizuri ya maisha yetu!

Mtangazaji la 1: Juma ijayo siku ya [TAJA SIKU] saa [TAJA SAA ZA KIPINDI] tutazungumzia kuhusu [TAJA MADA YA WIKI IJAYO]. Hadi wakati huo, kwaheri!

MUHTASARI WA KIPINDI

Kipindi kamili kuhusu mada ya 'Matumizi na Mabadiliko ya Tabia Nchi' saa 1



MAADILI NA IDHINI/ RUHUSA

Hii inaweza kuwa mada nyeti kwa wengine, kwa hivyo hakikisha umewafahamisha wasikilizaji wako kuwaheshimu wale watakaotoa simulizi zao za kibinafsi.

MUHTASARI WA KIPINDI

Kipengele Kijani - dakika 10



KUELEWA MATUMIZI NA MABADILIKO YA TABIA NCHI MWONGOZO WA SHUGHULI ZA KIJAMII

MAANDALIZI YA KIPINDI

MADA MAHUSUSI

NJIA TOFAUTI ZA KUZUNGUMZA KUHUSU MASOKO, MAVAZI NA MITINDO

- Jamii inyoasaidia kuweka thamani na kujifunza mbinu za kutengeneza mavazi kwa mikono
- Fikiria kuhusu alama ya athari zilizotokana na mavazi yako binafsi kutoka wakati wa kuzaliwa hadi sasa. Inaonekanaje?
- Mavazi yaliotengenezewa ndani kwa njia ya maadili. Hizi zinapatikanaje katika jamii yako?
- Viongozi wa vyombo vya habari vya kijamii: Je, wanaathirije maamuzi yetu ya ununuzi wa mavazi au bidhaa za aina fulani?
- Mzunguko wa maisha wa mavazi. Kutoka kwa mbegu hadi ifikiapo kutupwa kwa shimo kubwa la taka kwenye ardhi.
- Ni ishara gani hukuonya kwamba vazi fulani ni la mtindo wa haraka/kuharibu ardhi/kuathiri watu?

CHAGUA MADA MAHUSUSI

Viongozi wa vyombo vya habari vya kijamii (social media influencers): Wanathiri aje maamuzi yetu ya ununuzi wa mavazi au bidhaa za aina fulani?

Njia za kuzungumza kuhusu: Viongozi wa vyombo vya habari vya kijamii: Je, wanaathirije maamuzi yetu ya ununuzi wa mavazi au bidhaa za aina fulani?

- Viongozi wa vyombo vya habari vya kijamii (social media influencers) hushawishi tamaa yetu ya mitindo ya haraka.
- Je, kiongozi aliyewajibika hufanyaje? Ni nini haswa anasaidia kuuza?
- Kupenda kwetu kwa vitu - na shida inayoletea mazingira: vyombo vya habari vya kijamii na viongozi wa vyombo hivyo wanaweza kufanyaje?
- Vyombo vya habari vya kijamii ni chombo cha biashara kwa viongozi hao. Wasipouza mavazi na bidhaa, nao watatoa kipato chao wapi?

MUONGOZO WA SHUGHULI ZA KIJAMII

WIMBO MFUPI (JINGLE)

Lengo la winbo mfupi (jingle)
Jingle ni wimbo mfupi (au tune) ambao una ujumbe wazi na ni rahisi kuimba na kukumbuka.

MAHOJIANO

Lengo la mahojiano
Mahojiano ni mojawapo ya aina ya mazungumzo ambapo maswali huulizwa na mhojaji na majibu kutolewa na mhojiwa.

Maswali yaliyopendekezwa ya mahojiano na mmiliki wa biashara katika jamii:

- Alama ya kiikolojia ina maana gani kwako?
- Eleza uzoefu wako kwa “mitindo ya haraka”.
- Mawazo yako na tabia zako kuhusu mavazi zilikuaje wakati ulipoanza kujinunulia nguo?
- Zimebadilikaje tangu wakati huo?
- Katika jamii unayoishi, ni chaguo gani zilizopo za kuchakata mavazi, kununua nguo za mitumba au kununua mavazi kutoka kwa wabunifu wa ndani?
- Baadhi ya changamoto ambazo huwakabili vijana wakati wanapofanya maamuzi ya kununua mavazi ni kama gani?
- Ikiwa vijana wangetaka kujifunza zaidi kuhusu mzunguko wa maisha wa bidhaa, wanapaswa kwenda wapi?

MIUNDO YA VIPENGELE VYA KIPINDI CHA REDIO

MGENI (ALIYE NA UJUMBE MAALUM)

Lengo la kuwa na mgeni
Mgeni aliye alikwa ni mtu ambaye anaweza kushiriki kwa kutoa ujuzi wa kitaalam kuhusu taarifa ya athari au kutoa hadithi yake binafsi kuhusiana na taarifa ya athari.

Baadhi ya maswali ambayo mgeni anaweza kutafakari kabla ya mazungumzo:

- Kuna uhusiano upi kati ya masoko na mitindo?
- Je, vijana wanawezaje kufaidika kwa kuelewa mzunguko wa maisha wa mavazi wanayovaa au kununua?
- Ni mabadiliko gani makubwa katika tabia za vijana Watanzania ambayo wanahitaji kufanya kwa ununuzi wa mavazi?
- Vijana wanawezaje kuanza kupunguza mchangio wao kwa uharibifu wa dunia kupitia njia za ununuzi wao wa mavazi?

MCHEZO WA KUIGIZA

Lengo la mchezo wa kuigiza
Kutoa hali ambayo inaruhusu wasikilizaji “kuigiza” jambo kuhusu taarifa muhimu.

Chagua idadi ya wahusika wanaohitajika na wape waigize muongozo na fursa ya kutafsiri taarifa muhimu. Hili ni jambo ambalo waigizaji wenyewe watalifanya.

Waigizaji
Fatima, Maryam (rafiki wa dhati wa Fatima)

Maelezo ya hali
Fatima ana umri wa miaka 16. Anapenda kwenda kufanya manunuzi! Ni siku yake ya kuzaliwa na amebeba pesa zake kutembelea maduka ya ununuzi ili kujitunza mavazi mapya. Mara nyingi, yeye hununua nguo za mtindo kutoka kwenye duka maarufu sana la bei nafuu. Mavazi haya huchanika baada ya miosho michache tu. Lakini yeye anapenda kuvaa zilizo mtindoni, kwa hivyo anaona kuna thamani. Rafiki yake wa dhati, Maryam, hakubaliani na hayo. Anadhani ni athari kwa mazingira kuendelea kununua kutoka kwenye duka hili, na kumhimiza rafiki yake kuokoa fedha zake kwa manunuzi endelevu zaidi...

MIUNDO YA VIPENGELE VYA KIPINDI CHA REDIO

MAJADILIANO YA JOPO

Lengo la majadiliano ya jopo
Mjadala wa jopo unaohusisha kundi la watu kujadili mada moja mbele ya watazamaji. Kuna wakati wa maswali kutoka kwa watazamaji baadaye.

Watakao shiriki kwenye majadiliano ya jopo
Mtu anayefanya kazi katika biashara rejareja, kijana na mjasiriamali ambaye anauza mavazi yaliotengenezwa na mikono.

Mifano ya maswali ya kufungua mjadala wa jopo

- Je, alama ya kiikolojia ina maana gani kwako?
- Eleza uzoefu wako kwa “mitindo ya haraka”.
- Mawazo yako na tabia zako kuhusu mavazi yalikuaje wakati ulipoanza kujinunulia nguo?
- Yamebadilikaje tangu wakati huo?
- Katika jamii unayoishi, una chaguo gani za nguo za kuchakata mavazi, kununua nguo za mitumba au kununua nguo kutoka kwa wabunifu wa ndani?
- Baadhi ya changamoto ambazo vijana wanakabiliwa wakati wa kufanya maamuzi ya kununua mavazi ni zipi?
- Ikiwa vijana watataka kujifunza mengi zaidi kuhusu mzunguko wa maisha wa bidhaa, wanapaswa kwenda wapi?

JARIBIO

Lengo la jaribio
Kupima ujuzi wa msikilizaji wako kuhusu mada

Vitu unavyohitaji kwa zoezi hili
Maswali yaliyotayarishwa na majibu
Tuzo ndogo-ndogo

Mchakato
Wasilisha maswali na utoe tuzo kwa wale wapatao jibu sahihi.
Kutoka kwenye karatasi yenye habari zilizothibitishwa kuwa kweli, tumekuundia maswali mawili yafuatayo ili uyatumie kwenye kipindi chako. Baada ya kutumia haya mawili, jisikie huru kuunda maswali zaidi ili kuwapima wasikilizaji wako!

Jaribio 1
Swali: [.....] ni mambo yapi ambayo makampuni hufanya ili kufikia tamaa ya watumiaji na bidhaa ambazo hatuzihitaji, ili kupata faida kwao?
Jibu sahihi ni ‘masoko’ (marketing).

Jaribio 2
Mitindo ya haraka ni:
A. Unapo kula chakula kama vile burger wakati unapoendesha gari kwa kasi.
B. Viatu aina ya booti ambazo humwezesha mtu kutembea haraka ili usichelewe.
C. Mavazi ya bei nafuu, yasiyodumu.
Jibu sahihi ni C

MAANDALIZI YA SHUGHULI YA KIJAMII

Tumia miundo ya vipengele na utafiti wako wa kuandika muongozo wako. Hapa kuna mfano wa sehemu ya muongozo. Unaweza kuutumia kama mwongozo unapotayarisha maandalizi ya shughuli ya kijamii.

[MWANZO:]
Mtangazaji 1: Hamjambo na karibuni! Imetimia [TAJA SAA] na jina langu ni [TAJA JINA LAKO] kutoka [TAJA JINA LA KIKUNDI CHAKO]. Jiunge nasi wakati huu tunapozungumza kuhusu mada ambayo, pengine kwa njia moja au nyingine, imetuathiri sote.

Mtangazaji 2: Na jina langu ni [TAJA JINA LAKO]. Mimi ni [MWANAHABARI KIJANA/MTOTO] kutoka kwa [TAJA JINA LA KIKUNDI CHAKO] na makala yetu ya leo inaangazia jinsi vijana wanaweza kufikia rasilimali na kuendeleza ufahamu kuhusu jinsi wanavyoweza kupunguza athari yao ya kwenye mazingira kwa kupunguza kiasi cha mavazi taka kwenye duniani. Vipi? Tutaweza kupiga mbizi kwa undani ili kujua jinsi na kwa nini katika majadiliano haya. Lakini pia tunataka kusikia kutoka kwako!

Mtangazaji 1: Hiyo ni kweli! Tutazungumza kuhusu umuhimu wa vijana kutochangia kujaza mashimo makubwa ya taka kwenye ardhi kwa kununua mavazi mapya kila mwezi mitindo inavyobadilika. Au kutupa nguo za zamani badala ya kuzichakata.

Mtangazaji 2: Hiyo ni kweli, tutazungumzia pia kwa nini ni muhimu sana kwamba vijana, na watu wote, wazingatie jinsi wanavyojali nguo, kutoka wakati wanapozinunua hadi wanapozichoka na kuzitupa. Mahitaji ya nguo kwa Watanzania yanakuwa kwa haraka sana. Bila mabadiliko katika tabia zetu kama watumiaji, sekta ya nguo inaweza kutumia hadi 26% ya bajeti ya kaboni duniani kwa mwaka wa 2050.

Mtangazaji 1: Wow! Hiyo inamaanisha tungechangia 2% kwa kuongezeka kwa kiwango cha joto ulimwenguni. Sio poa! Leo, tutaangazia watu wanaonunua, kuuza na kuvaa mavazi katika jamii yetu. Karibu kila mtu huvaa nguo, lakini ni wangapi wetu wanaojua safari ambayo mavazi hayo yamepita ili kutufikia? Na ni wangapi wetu wanaofikiria watakavyo zitupa wakati hatuzitaki au kuzihitaji tena. Ili kufanya hivyo, tunashirikisha sauti za jumuiya yetu kutuambia jinsi vyombo vya habari vya kijamii, matangazo na bidhaa zinatumiwa na watu wote, wadogo kwa wazee, katika maisha yetu ya kila siku. Tunakuletea habari zinazohitajika ili kuanza mazungumzo ya wazi kuhusu masoko, mavazi na mitindo.

Mtangazaji 2: Hebu tusikie zaidi kile ambacho watu wanafikiri kuhusu masoko, mavazi na mitindo. [SHIRIKISHA WANAOHUDHURIA/WANAOSIKILIZA KWA KUULIZA MASWALI NA KUWAPA FURSA YA KUTOA MAONI YAO WAZI].

Mtangazaji 1: Wow! Hiyo ilikuwa taarifa ya kuvutia sana! Kuna mengi zaidi kwa masoko na ulimwengu wa mavazi kuliko tunavyofikiri.

Mtangazaji 2: Hasa kabisa! Sisi, kama vijana, tuna haki ya kupata habari ambazo zinaweza kutufaidi na kutupatia ustawi wetu leo na siku zijazo. Hebu tafakari kuwa na ujuzi wa viwanda vya mavazi, mitindo ya haraka na hata mengi zaidi!

Mtangazji 1: Hakika! Sasa hebu tupate maelezo zaidi kutoka kwa mgeni wetu wa leo ambaye ni mbunifu wa nguo. Atatusaidia kuelewa zaidi kuhusu kutengeneza mavazi ambayo hayaathiri dunia (eco-friendly). Pia atazungumzia maneno haya [alama za kimazingira - egological foortprint]. Baadaye, tutakuwa na jaribio kuhusu neno hilo na mengi zaidi! Usiondoke!

[FUNGUA KIPENGELE CHA MAZUNGUMZO NA MGENI MAALUM]
[CHEZA MAZUNGUMZO NA MGENI MAALUM/MPE FURSA YA KUZUNGUMZA]
[FUNGA KIPENGELE CHA MGENI MAALUM]

MAANDALIZI YA SHUGHULI YA KIJAMI



MAADILI NA IDHINI/ RUHUSA

Hii inaweza kuwa mada nyeti kwa wengine, kwa hivyo hakikisha umewafahamisha wasikilizaji wako kuwaheshimu wale watakaotoa simulizi zao za kibinafsi.

Baada ya kukamilisha muongozo wako, kupanga wasanii wako, kuandaa shughili ya kijamii na miundo yote, ni wakati wa kuanza!